TANGAZO LA SERIKALI NA. 179 la tarehe 8/3/2019

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

(*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)*)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA ZA MWAKA 2019

## SEHEMU YA I
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina la sheria

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga za Mwaka, 2019.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali, ruhusa ya kufanya biashara au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, isipokuwa mkokoteni

au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo;

“Halmashauri“maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

“kibali cha uendelezaji” ni kibali kinachotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia kifungu cha 29(1) cha Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya Mwaka 2007;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“mkusanyaji ushuru” maana yake ni mtumishi wa Halmashauri au mtu mwingine yeyote au kikundi aliyeteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri;

“nyumba za Halmashauri’ maana yake ni nyumba zinazomilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwa ajili ya biashara au kupangisha au nyumba kwa ajili ya makazi zinazotumiwa na watumishi wa Halmashauri;

“stendi” maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia au kuteremsha abiria au mizigo ya abiria hii itajumuisha pia kituo cha kupaki malori na vituo vingine vidogo vidogo vya kupakia na kushusha abiria vya Halmashauri;

“usajili wa vyombo vya usafiri**”** maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri ;

“ushuru*”*maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala kwa ajili ya huduma, mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

## SEHEMU YA II
### ADA NA USHURU

Mamlaka ya Halmashauri kutoza ada na ushuru.

4.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na ushuru utakaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa.

Ushuru wa huduma

5.-(1) Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kwa kila mfanyabiashara anayepaswa kuwa na leseni ya biashara, Kampuni au Taasisi ya biashara katika kila mwaka na mapato ambayo ni sawa na asilimia sifuri nukta tatu (0.3) ya hesabu ya shughuli zote zikiwemo za uuzaji au uzalishaji wa bidhaa au huduma kutoka nje ya Nchi zinazofanyika katika eneo la Halmashauri ukiondoa Kodi ya Ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa;

(2) Ushuru wa huduma itatozwa kwa mtu, kampuni au taasisi bila kujali mahali ilipo makao makuu ya biashara ya mlipa kodi huyo.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru.

6.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa ada na ushuru kuhakikisha kwamba analipa kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi;

(2) Muda wa kukusanya Ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili (12;00) kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili (12;00) kamili jioni;

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2), Maafisa wa Halmashauri au Wakala anaweza kukusanya Ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu endapo atakuwa na kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa;

(4) Malipo ya Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au

kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na Mlipa Ushuru;

(5) Malipo ya ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielekitroniki itakayothibitisha ulipaji wa malipo hayo;

Uteuzi wa wakala

7.-(1) Halmashauri inaweza kuteua Kampuni, Asasi, au taasisi yoyote kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika vyanzo vilivyokubaliwa kukusanywa na Wakala;

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:-

(a) kukusanya ushuru katika eneo na chanzo alichopangiwa viwango vilivyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti mkataba wa uwakala kati yake na Halmashauri.

Ukusanyaji wa madeni

8.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu au taasisi itakuwa imeshindwa kulipa ada na ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 8(1) hapo juu, Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya Ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za wadaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini (30) kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri Masharti yaliyowekwa katika kifungu

kidogo cha (3) na (4), Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri,isipokuwa kama hasara hiyo itakua imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Uwezo wa Afisa Mwdhiniwa

9.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa;-

(a) kuingia katika jengo lolote kwa lengo la kukusanya ushuru.

(b) kukagua eneo au chombo chochote atakachokitilia mashaka kuwa kinahifadhi au kusafirisha bidhaa au kinatumika kukwepa kulipa ushuru.

## SEHEMU YA III
### MAKOSA NA ADHABU

Makosa

10. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(1) Kwa wakala endapo;

(a) atakusanya Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba kutoka kwa Halmashauri;

(b) atajaribu au atakusanya ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo hizi;

(c) atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

(d) atakusanya ushuru kwa mbinu tofauti na alizoelekezwa na Halmashauri.

(2) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi endapo;-

(a) atashindwa, atadharau, atakaidi au atakataa kulipa ada na ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada na ushuru

chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa ada na ushuru;

(c) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au utunzaji wa nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada na ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au atashindwa kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yeyote yatakayohitajika na Halmashauri;

(f) atamzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake;

(g) atafanya bila kibali au leseni biashara au shuguli yoyote inayotakiwa kulipiwa leseni au kibali kinachotakiwa kulipiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(h) atafanya biashara katika eneo lisiloruhusiwa au ambalo halikutengwa na Halmashauri;

(i) atakataa kuonyesha risiti aliyolipia ushuru kwa Afisa Mwidhiniwa au kwa wakala;

Adhabu

11. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000) au Kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha

12. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini

kosa

isiyopungua shilingi laki mbili (200,000) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama ilivyoelekezwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Tangazo la Serikali Na. 173 la tarehe 26/9/2008

13. Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko) za Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga,2008.

SEHEMU YA IV
JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 4(1)*

(a) Ushuru wa kukodisha mali za Halmashauri.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba za Halmashauri kwa ajili ya biashara | Kwa kuzingatia mkataba. |
| 2 | Ukumbi mkubwa wa mikutano(daraja la tatu) | 200,000/= kwa siku |
| 3 | Ukumbi mkubwa wa mikutano (daraja la pili) | 400,000/= kwa siku |
| 4 | Ukumbi mkubwa wa mikutano (daraja la kwanza - VIP) | 1,000,000/= kwa siku. |
| 5 | Ukumbi mdogo wa mikutano | 150,000/= kwa siku |
| 6 | Meza 1 ya mikutano | 500 kwa siku |
| 7 | Kiti 1 | 300/= kwa siku |
| 8 | Gari la maji taka | 50,000/= kwa trip moja |
| 9 | Gari la mizigo linapokodiwa na watu binafsi (Ujazo wa Mita za mraba 1-5 ) | 60,000/= kwa trip moja. |
| 10 | Gari la mizigo linapokodiwa na watu binafsi (ujazo wa mita za mraba 5-8) | 200,000/= kwa trip moja. |
| 11 | Magari mengine ambayo hayajatajwa | 300,000/= kwa siku |
| 12 | Gari la mizigo linapokodiwa na wakandalasi kwa mafuta na dereva wao. | 500,000/= kwa saa 8 kwa ujazo wowote. |
| 13 | Mgahawa wa chakula. | Kwa kuzingatia mkataba |
| 14 | Kukodisha ofisi | Kwa kuzingatia mkataba |
| 15 | Mali zingine ambazo hazijatajwa | Kwa kuzingatia mkataba. |

SEHEMU YA PILI

(b) Ushuru/kodi ya kupangisha vibanda au vyumba vya Halmashauri.

| NA | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Soko kuu | Kwa kuzingatia kiwango kilichoainishwa kwenye mkataba. |
| 2 | Soko Matola/stendi kuu | Kwa kuzingatia kiwango kilichoainishwa kwenye mkataba. |
| 3 | Soko la Mandela | Kwa kuzingatia kiwango kilichoainishwa kwenye mkataba. |
| 4 | Masoko mengine ambayo hayakutajwa | Kwa kuzingatia kiwango kilichoainishwa kwenye mkataba. |

(c) Ada na ushuru wa mazao.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mazao ya mahindi, mchele au mpunga, mhogo mkavu, mtama,uwele,ulezi, karanga, alizeti, ngano, shayiri ufuta na Mazao ya biashara ya kimkakati kama tumbaku, kahawa, pamba,chai, kakao,mpira,miwa,korosho, katani | Asilimia tatu (3%) ya bei ya soko. |
| 2 | Mazao yaliyochakatwa na kuongezewa thamani na au mabaki ya mazao. | Asilimia tatu (3%) ya bei ya soko. |
| 3 | Mazao ya mizizi, matunda pamoja na Mazao mengine ambayo hayajatajwa. | asilimia tatu ( 3%) ya bei ya soko. |

(d) Ada ya usajili wa vyombo vya usafiri wa Halmashauri.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mabasi madogo au daladala | 30,000/= kwa mwaka |
| 2 | Teksi | 20,000/= kwa mwaka |
| 3 | Bajaji | 15,000/= kwa mwaka |
| 4 | Bodaboda | 10,000 /=kwa mwaka |
| 5 | Magari ya mizigo yanayokodiwa. | 50,000/= kwa mwaka |
| 6 | Magari madogo ya kukodiwa maarufu kama kirikuu. | 30,000 /= kwa mwaka |

(e) Ada na ushuru wa mifugo.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Kibali cha kusafirisha mifugo (Ndani ya Halmashauri) | Kwa kuzingatia mwongozo wa Wizara ya kisekta na Sheria iliyotungwa na Bunge. |
| 2 | Kibali cha kusafirisha mifugo (Nje ya Halmashauri) | Kwa kuzingatia mwongozo wa Wizara ya kisekta na Sheria |

*Tangazo la Serikali Na. 179 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | | iliyotungwa na Bunge. |
| 3 | Faini ya wanyama wanaozurura ovyo | 50,000/= kwa mnyama |
| 4 | Ushuru wa kuhifadhi wanyama waliokamatwa wakizurura ovyo. | 10,000/= kwa siku. |
| 5 | Ushuru wa mnada wa ng’ombe na punda | 5,000/=kwa mnyama mmoja |
| 6 | Ushuru wa mnada wa mbuzi, kondoo na nguruwe na wanyama wengine. | 1,500/=kwa mnyama mmoja |
| 7 | Ada ya machinjio ya ng’ombe na punda (isiyohusisha gharama za kuchinja) | 5,500/= kwa mnyama mmoja |
| 8 | Ada ya machinjio ya mbuzi, kondoo, nguruwe na wanyama wengine. (isiyohusisha gharama za kuchinja) | 2,000/=kwa mnyama mmoja |
| 9. | Faini ya kuchinja nje ya machinjio | 50,000/= |
| 10. | Ada ya huduma ya chanjo ya mifugo mikubwa (ng’ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe) | Kwa kuzingatia mwongozo na Wizara. |
| 11. | Ada ya huduma ya chanjo ya mifugo jamii ya ndege (kuku, kanga, bata bata mzinga) | Kwa kuzingatia mwongozo wa Wizara. |
| 12. | Ada ya chapa ya mifugo | Kwa kuzingatia mwongozo wa Wizara |
| 13. | Ada ya huduma ya chanjo ya mbwa | Kwa kuzingatia mwongozo wa Wizara |

(f) Ada na ushuru wa stendi kubwa na stendi ndogo zilizotengwa.

| Na. | Aina ya chanzo | Kiasi . |
|---|---|---|
| 1 | Mabasi makubwa zaidi ya abiria 45 | 5,000 /=kila yanapotoka na abiria. |
| 2 | Mabasi chini ya abiria 45 | 3,000 /=kila yanapotoka na abiria |
| 3 | Mabasi ya abiria chini ya 25 | 2,000/= kila yanapotoka na abiria. |
| 4 | Bajaji inayoingia stendi | 2,000 /=kwa siku. |
| 5 | Boda boda inayoingia stendi | 1,000/= kwa siku |
| 6 | Mkokoteni unaoingia stendi | 1,000/= kwa siku |
| 7 | Magari ya binafsi na teksi | 500 /=kila inapoingia. |
| 8 | Magari ya stafu wa stendi wenye kitambulisho rasmi | 1,000 /=kwa siku |
| 9 | Ushuru wa wasindikizaji yaani wasiokua abiria isipokuwa wadau wa stendi wenye vitambulisho. | 200/= kila anapoingia. |

(g) Ada ya Maegesho Maeneo maalum yaliyotengwa na Halmashauri na ushuru wa kuingia na kushusha mizigo mjini.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Magari chini ya tani 7 | 5,000/= kwa siku |
| 2 | Magari ya tani 7 - 20 | 10,000/= kwa siku |
| 3 | Magari mengineyo | 5,000/= kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Faini ya gari ya kuanzia tani 20 linapoegeshwa eneo lisilo maalum (eneo ambalo halikutengwa na Halmashauri). | Kwa kuzingatia faini inayotajwa katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290 kadri itakavyorekebishwa. |
| 5 | Ushuru wa kushusha na kupakia mizigo katika eneo la mjini kwa gari la kuanzia tani 7. | 100,000/= kwa tripu moja. |
| 6 | Usajili wa maegesho ya magari binafsi | 1,000,000/= kwa mwaka |
| 7 | Ushuru wa Halmashauri katika maegesho ya magari binafsi (inalipwa na mmiliki wa maegesho) | 5,000/= kwa siku |

(h) Ada na ushuru wa kusafirisha madini ya ujenzi.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Uzito wa gari ya tani 1 - 3 | 5,000/= kwa tripu moja |
| 2 | Uzito wa gari tani 4 - 7 | 10,000/= kwa tripu moja |
| 3 | Uzito tani 8 – 20 | 30,000/= kwa tripu moja |
| 4 | Kibali cha kufanya shughuli za kuchimba michanga kwa ajili ya ujenzi maeneo maalum, kufyatua tofali za kuuza maeneo maalum na kuuza tofali. | 30,000/= kwa mwaka |

(i) Ada ya kuendesha shughuli za utamaduni, burudani na michezo.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Kibali cha ngoma za jadi na matamasha kama hayo. | 50,000/= kwa onyesho moja. |
| 2 | Kibali cha disco, maonyesho ya bendi, cinema na matamasha makubwa ya muziki na mashindano mbalimbali ya michezo na ulimbwende(yanapofanyika ukumbini) | 150,000/= kwa onyesho moja la kukesha. |
| 3 | Kibali cha disco, maonyesho ya bendi, cinema na matamasha makubwa ya muziki na mashindano mbalimbali ya michezo na ulimbwende(yanapofanyika uwanjani) | 300,000/= kwa onyesho |
| 4 | Ada ya kumbi za usiku/night clubs, casino (idhini ya kukesha) | 1,000,000 /=kwa mwaka. |
| 5 | Ada ya kufanya mnada wa hadhara kwa matangazo na promosheni mbalimbali za bidhaa zinazoweza kukusanya watu eneo la wazi au sokoni. | 50,000/= kwa siku. |
| 6 | Kibali cha kuendesha shughuli ya kukodisha kumbi au shughuli za ukumbini, kumbi za video na maonyesho ya mpira ya usiku. | 100,000/= kwa mwaka |

*Tangazo la Serikali Na. 179 (linaendelea)*

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 7 | Matamasha ya mziki wa nyimbo za dini yanapofanyika uwanjani au ukumbini kwa kiingilio. | 100,000/= kwa onyesho moja la ukumbini.<br>150,000/= kwa onyesho la uwanjani |
| 8 | Ada ya waganga wa jadi waliosajiliwa au wataalam wa tiba mbadala waliosajiriwa. | 100,000/= kwa mwaka |
| 9 | Ada ya kuweka mashine za bahati nasibu ndani ya eneo la Halmashauri kwa mwenye leseni ya bodi ya bahati nasibu pekee. | 1,000,000/= kwa mwaka |
| 10 | Matangazo yakutumia vipaza sauti | 50,000/= kwa siku |
| 11 | Usajiri wa vikundi vya sanaa na michezo (vyama vya michezo), vituo vya michezo, gymnasium, ada ya pray stations, kuchezesha pool table, kibali cha kusajili wa washereheshaji (mc) au dj's, (isipokuwa katika misiba na maafa na tafrija ndogo zinapofanyika nyumbani) vikundi mbalimbali. | 100,000/= kwa mwaka |
| 12 | Kibali cha 'l*ocation*' za video, filamu, sinema kwa wasanii wasio wakazi wa Halmashauri. | 5,000/= kwa '*location'* |
| 13 | Kibali cha kukesha baa au maeneo mengine ya starehe na yanayouza vileo. | 50,000/= kwa siku. |
| 14 | Kibali cha kuuza chips, mgahawa kwa kukesha. | 30,000/= kwa siku |
| 15 | Kibali cha kukesha kwa sherehe. | 50,000/= kwa siku |
| 16 | Kibali cha kufunga mtaa au eneo la wazi kwa ajili ya sherehe wakati wa mchana (isipokuwa sherehe za kidini zinazotambulika) | 100,000 /=kwa siku. |

(j) Ushuru wa magulio na minada.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa ndani ya soko kwa meza | 300/= kwa siku |
| 2 | Ushuru wa magulio kwa meza | 300/= kwa siku |
| 3 | Ushuru wa wauza mitumba, nguo, viatu na bidhaa zingine za kuvaliwa wanapokuwa gulio au mnada usio soko lao la kila siku. | 500/= kwa siku |
| 4 | Watoa huduma ya chakula ndani ya soko | 200/= kwa siku |
| 5 | Kuuza pombe za asili gulioni au mnadani | 1000 /= kwa siku |
| 6 | Kuuza pombe za kigeni gulioni au mnadani | 2,000/= kwa siku |
| 7 | Biashara nyingine yoyote ikiwa gulioni au mnadani | 1000 /= kwa siku |

(k) Ada na ushuru wa mazao ya misitu.

| Na | Aina ya chanzo | Ushuru/ada/tozo |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Miti ya mirunda | 100/= kwa mrunda mmoja. |
| 2 | Mzigo wa Kuni | 6,000/= kwa tani moja. |
| 3 | Gunia moja la mkaa | 12500/= kwa gunia moja. |
| 4 | Kibali cha kituo cha kuuza mbao, miti, magogo, nguzo za miti na mkaa kwa mwenye kibali kutoka kwa Wakala wa Misitu Tanzania | 50,000/= kwa mwaka |
| 5 | Ubao bila kujali unene | 150/= kwa ubao bila kujali ukubwa. |
| 6 | Nguzo bila kujali unene | 1,000/= kila nguzo moja. |
| 7 | Kibali cha shughuli za useremala | 30,000/= kwa mwaka. |
| 8 | Kibali cha kiwanda kidogo cha mbao (chenye mashine ya umeme) chenye kibali kutoka Wakala wa Misitu Tanzania | 150,000/= kwa mwaka |
| 9 | Ushuru wa kuuza asali, nta na mazao mengine ya nyuki | 200/= kwa siku. |
| 10 | Kibali cha kukata mti. | 10,000/= kwa mti mmoja |
| 11 | Kibali cha kusafirisha mazao ya misitu (ambayo hayajalipiwa yalikotoka au yanayotoka ndani ya Halmashauri) | 20,000 /= |
| 12 | Ushuru wa Mazao mengine yote. | 500/= kwa siku. |

(l) Ushuru wa biashara za samaki.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Leseni ya biashara ya samaki na mazao ya majini. | 10,500/= kwa mwaka. |
| 2 | Ushuru wa dagaa wanaouzwa jumla kwa walanguzi | 100/= kilo moja. |
| 3 | Ushuru wa samaki wanaouzwa jumla kwa walanguzi | 400/= kwa kilo moja |
| 4 | Kiwanda cha samaki na mazao mengine ya majini inaposafirishwa nje | 50,000/= kwa kila tani moja. |
| 5 | Kiwanda cha samaki na mazao mengine ya majini inapouzwa ndani ya nchi. | 20,000/= kwa kila tani moja. |

(m) Ushuru wa usafi na mazingira.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Makazi ya watu binafsi(kaya) | 1,000/= kwa mwezi |
| 2 | Kiwanda kidogo cha mbao, fundi seremala, vibanda umiza na vibanda vya chips, karakana mbalimbali, bucha za nyama na samaki, maduka ya rejareja, vibanda na viziba vya sokoni. | 2,000 /=kwa mwezi |
| 3 | Migahawa midogo | 2,000 /= kwa mwezi |
| 4 | Nyumba za kulala wageni, hotel, duka la jumla, baa, grocery, club za pombe za asili, stoo za mkaa, mbao ,gereji, sehemu za kuosha magari, godown, stoo, | 5,000/= kwa mwezi |

*Tangazo la Serikali Na. 179 (linaendelea)*

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| | kiwanda kikubwa cha mbao, club za usiku, kasino. | |
| 5 | Aina nyingine za biashara ambazo hazijatajwa | 1,000/= kwa mwezi. |
| 6 | Maeneo yanayotoa huduma za kijamii kama afya, elimu, vituo vya malezi, maeneo ya kuabudia na taasisi za serikali. | 1,000/= kwa mwezi. |
| 7 | Maeneo ya vituo vya mafuta, viwanda ambavyo leseni za biashara hazitolewi na Halmashauri, super market, kampuni inayofanya shughuli za ujenzi wa barabara, madaraja au Majengo makubwa unaoendela, , maegesho ya magari binafsi. | 10,000/= kila mwezi |

(n) Ada ya upimaji ardhi na vibali vya ujenzi.

| Na | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Kibali cha ujenzi nyumba ya makazi isiyo ghorofa | 30,000/= |
| 2 | Kibali cha ujenzi nyumba ya makazi na biashara | 45,000/= |
| 3 | Kibali cha ujenzi nyumba ya kuabudia | 20,000 /= |
| 4 | Kibali cha ujenzi wa ghala | 50,000 /= |
| 5 | Kibali cha ujenzi wa ukuta au fensi | 20,000 /= |
| 6 | Kibali cha ujenzi wa vibanda vidogo. | 10,000 /= |
| 7 | Kibali cha ujenzi ghorofa – makazi | 100,000 /= |
| 8 | Kibali cha ujenzi ghorofa – biashara | 200,000 /= |
| 9 | Kibali cha ujenzi shule binafsi, vituo vya kulelea watoto na makundi maalum, zahanati, kituo cha afya. | 45,000 /= |
| 10 | Kibali cha ujenzi jengo lolote la serikali lisilomilikiwa na Halmashauri ya Manispaa. | 20,000 /= |
| 11 | Kibali cha ujenzi wa choo cha kulipia | 50,000/= |
| 12 | Kibali cha ujenzi wa kitu kingine chochote ambacho hakijatajwa. | 20,000 /= |
| 13 | Kibali cha ujenzi wa minara ya mawasiliano, gereji bubu,car wash. | 50,000 /= |
| 14 | Ada ya kibao cha namba ya nyumba,jengo lolote lililokwisha jengwa na kukamilika. | 2,000 /= |
| 15 | Kibali cha kuita jina la mtaa litakalokubaliwa na wana mtaa mtu binafsi. | 5,000,000/= |
| 16 | Ada ya ukaguzi eneo la ujenzi | 10,000 /= |
| 17 | Leseni za makazi. | 30,000 /= |
| 18 | Faini ya kujenga bila kibali cha ujenzi. | 2% ya thamani ya jengo. |
| 19 | Ada ya kufufua mipaka ya kiwanja | 20,000/= |
| 20 | Ada ya kibali cha upimaji viwanja au urasimishaji kwa kampuni binafsi iliyokidhi vigezo. | 10% ya fedha yote atakayopata kabla ya kutoa gharama za kodi. |

(o) Ada na ushuru mbalimbali.

| Na. | Aina ya chanzo | Kiasi |
|---|---|---|

*Tangazo la Serikali Na. 179 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Kulipia mnara wa simu, redio na minara au nyaya za mawasiliano mengine katika eneo linalomilikiwa na Halmashauri/Kijiji. | Kwa kuzingatia mkataba. |
| 2 | Kulipia mnara wa simu, redio na minara au nyaya za mawasiliano mengine katika eneo linalomilikiwa na mtu binafsi au taasisi nyingine yoyote (kulipwa na mmiliki wa eneo) | 5% ya bei ya makubaliano ya mwaka mmoja. |
| 3 | Ushuru wa Choo cha kulipia | 200/= haja ndogo<br>300/= haja kubwa<br>500 kuoga |
| 4 | Ada na ushuru wa upimaji wa afya wahudumu wa bar, hotel na nyumba za kulala wageni | 10,000 /= kwa mtu (kwa miezi sita) |
| 5 | Ushuru wa hoteli zote zinazotafsiriwa kuwa nyumba za kulala wageni chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa sura ya 290 | 10% ya fedha anayolipa mgeni kwa siku. |
| 6 | Kibali cha uendelezaji (Development charge) shughuli za ujenzi wa barabara au uchimbaji wa madini. | 200,000/= |
| 7 | Ushuru wa mwalo mdogo wa kuchengua madini, krasha la kusaga mawe ya madini au mawe mengine ya kawaida. | 1,000,000/= kwa mwaka. |

JEDWALI LA PILI
HATI YA KUKIRI KOSA
(*Chini ya Kifungu cha 12*)

Mimi…. ………………………..…………………………………………………… nakiri mbele ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, kwamba, mnamo tarehe ……. ya mwezi ……… mwaka ………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ………… cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga za mwaka 2019.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, kwa hiyari yangu niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru unaodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu na ufahamu wangu.

Leo tarehe ……………………………… ya mwezi …………………………..… mwaka ………..……
Jina……………..………………...…………………………
Saini…………………………….…………………………

Mbele ya:
Jina………………………………………………….
Cheo ………………………………………………..
Saini …………………………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 2 ya mwezi Septemba, mwaka 2018.

JACOB J. MTALITINYA
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Manispaa*
*Sumbawanga*

JASTIN E. MALISAWA
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Manispaa*
*Sumbawanga*

NAKUBALI

Dodoma,
11 Februari, 2019

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*WN-OR-Tamisemi*